




Panua mustakabali wako kifedha



 **FinScope**
TANZANIA 2013

UTANGULIZI

FinScope Tanzania 2013 ni mzunguko wa tatu wa utafiti wa kutambua na kupima mahitaji na upatikanaji wa huduma za fedha miongoni mwa watu wazima waishio Bara na Zanzibar. Taarifa za utafiti huu zina umuhimu mkubwa kwa maendeleo yahasuyo upatikanaji wa huduma jumuishiki za fedha: zinabainisha huduma zinazotumiwa na zisizotumiwa na watu pamoja na sababu zake; vikwazo vya matumizi zaidi ya huduma hizo, na tofauti zinazojibainisha kati ya mkoa na mkoa. Utafiti huu pia unatoa mwanga kuhusu mitazamo na mienendo ya watu, kuhusu tofauti zao kijinsia, kuhusu maeneo ya mijini na vijijini, mwuelekeo na uwigo wa kuchagua - vyote hivyo vikiwa kwenye mtazamo uliodumu kwa miaka saba sasa.

Utafiti wa kwanza wa FinScope Tanzania ulifanyika mwaka 2006, ukifuatiwa na wa pili mwaka 2009. Watu wazima 8,000 (wenye umri wa zaidi ya miaka 16) walishiriki katika utafiti huu kama sampuli ya kitaifa ya watu wote wazima. Kutokana na aina hii ya utafiti kuwa umefanyika katika nchi nyingi za Afrika, FinScope Tanzania inaweza kutoa ulinganifu mwaafaka kati ya Tanzania na mataifa mengine katika bara hili.

Utafiti huu ni wa muhimu sana kwa taasisi za umma na binafsi kama vile: wizara, Benki Kuu ya Tanzania, tasnia ya huduma za fedha, kampuni zikwa simu za mkononi, washirika wa maendeleo, vyuo vikuu, asasi za utafiti, asasi zisizo za kiserikali na asasi za kiraia.

SAMPULI

Shabaha ya Sampuli

Maeneo 800 ya kiuchunguzi, kila eneo mahojiano 10

Jumla – mahojiano 8,000



walihojiwa katika mikoa
yote ya Bara na Zanzibar

Sampuli iliyofikiwa:

Mahojiano 7,987

Mwitikio:

99.8%

Data linganifu / zilizo husianishwa:

Watu wenye umri wa miaka 16 au zaidi –
m 24.2 (m 21.2 mwaka 2009)

Watu wenye umri wa miaka 18 au zaidi –
m 23.2 (m 20.0 mwaka 2009)

Ni muhimu kuzingatia kuwa chati zote za mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha za mwaka 2009 zimekokotolewa upya kwa kutumia tafsiri ya mwaka 2013. Maelezo kamili ya tafsiri zote yameorodheshwa mwishoni mwa kijitabu hiki.



IDADI YA WATU

Mgawanyo watu Mijini / Vijijini nchini kote



MIJINI



33.8%



66.2%



VIJIJINI



Msingi: jumla kuu ya watu wazima

Kuhama kwa watu kutoka maeneo ya vijijini kwenda mijini kunaendelea kuongezeka Bara, lakini ni kwa kiasi kidogo kwa upande wa Zanzibar. Hata hivyo theluthi mbili ya watu wote bado wapo maeneo ya vijijini; kuna wanawake wengi kidogo kuliko wanaume nchini kote na kundi kubwa la watu ni wenye umri kati ya miaka 21 na 30.

Viwango vya elimu

Wasio na elimu rasmi



Zaidi ya elimu ya msingi/sekondari



Zaidi ya Elimu ya sekondari



Elimu ya msingi au chini


Elimu inabakia kuwa ni eneo la kutiliwa maanani kwa kiasi kikubwa. Watoaji wa huduma za fedha katika makundi yote wanatakiwa kutoa bidhaa/huduma kwa kutambua viwango vya chini vya elimu vya wateja walio wengi. Kama chati hii inavyoonyesha, theluthi mbili ya watu wazima wanaelimu ya msingi pekee - takwimu ambayo kimsingi haijabadilika tangu 2006.




Msingi: jumla kuu ya watu wazima

KIPATO

Chanzo kikubwa cha fedha



 % watu wazima 2013

Msingi: jumla kuu ya watu wazima


Karibu robo ya watu wote (5,554,717) ni wategemezi kwa wengine kama chanzo chao cha kipato. Idadi ya watu ambao chanzo chao cha mapato kinatokana na ajira rasmi inabakia kuwa ndogo (1,099,612 au 4.5%).

FinScope inaonyesha jumla ya waajiriwa rasmi kama 1,242,724 (5.1%), idadi ambayo karibu ni sawa na takwimu zilizotolewa na Wizara ya Kazi na Ajira.



MPANUKO WA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA FEDHA

Upatikanaji Bara na Zanzibar



Chanzo: jumla kuu ya watu wazima


Chati za 2009 zimekokotolewa upya kwa kutumia tafsiri za mwaka 2013 za Mpanuko wa upatikanaji wa Huduma za Kifedha

Zanzibar bado iko nyuma ya Bara kwa maana ya watu wasio tumia kabisa huduma za fedha. Tofauti kubwa zaidi tangu 2009 ni kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotumia huduma kutoka Taasisi Rasmi Zisizo Benki. - hasa huduma kwa simu za mkononi. Hata hivyo, watu kwa upande wa Zanzibar wamekuwa wazitosiyo wepesi kuchangamkia fursa hii. Ni moja ya tano pekee ya watu wazima kwa upande wa Zanzibar ndiyo mpaka sasa wameweza kuchangamkia huduma za fedha kwa simu za mkononi, ukilinganisha na karibu nusu kwa upande wa Bara.

Ingawa kwa sasa nchini kuna benki tofauti zipatazo hamsini, ikiwa ni ongezeko la benki kumi na moja zaidi tangu 2009 - kuna ongezeko dogo tu la jumla ya idadi ya watu wazima wanaotumia huduma za benki kwa upande wa Zanzibar na Bara.




Ulinganisho wa mpanuko wa upatikanaji wa huduma za kifedha 2009 & 2013, wanawake & wanaume



Kuna ongezeko dogo katika matumizi ya bidhaa/huduma za benki japo ongezeko hilo ni dogo kwa wanawake kuliko kwa wanaume. Hata hivyo kuna ongezeko kubwa na la ghafla katika kutumia huduma rasmi zisizo za benki - mara nyingi, zikiwa ni huduma kwa simu za mkononi - kwa wote wanaume na wanawake. Matokeo yake, kumekuwa na kupungua kwa matumizi ya huduma zisizo rasmi na kiwango cha wale wasiotumia huduma yoyote ya fedha.

Ulinganisho wa mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha 2009 & 2013, mijini/vijijini




Kinachovutia na cha pekee zaidi kuhusu FinScope 2013 ni taarifa ya kuongezeka kwa uwiano wa watu wazima wenye au wanaotumia huduma rasmi zisizo za benki. Mabadiliko haya ndiyo yaliyosababisha kupungua kwa idadi ya watu wasiotumia huduma yoyote ya fedha. Matumizi yanayotegemea njia au taratibu za huduma za fedha zisizo rasmi pekee yamepungua sana katika maeneo ya mijini, na kidogo zaidi katika maeneo ya vijijini.

Katika chati hizi, kila mshiriki wa utafiti anahesabiwa katika kundi moja tu. Washiriki wanatokea mara moja tu: iwapo wanatumia huduma rasmi za asasi zisizo benki au huduma zisizo rasmi lakini pia hutumia huduma rasmi za benki, watahesabiwa tu katika kundi la huduma rasmi; la Benki; iwapo wanatumia huduma zote mbili: rasmi zisizo za benki na zisizo rasmi, wataingizwa katika kundi la huduma rasmi zisizo za benki.


Ulinganisho wa mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha kwa chanzo kikuu cha mapato

Walioajiriwa au kujijiri katika kilimo wanayo nafasi ndogo ya kutumia bidhaa na huduma za benki, ingawa upatikanaji wa huduma za fedha kwa simu za mkononi umekuwa wa msaada mkubwa kwao. Zaidi ya robo tatu ya walioajiriwa katika sekta rasmi wanatumia huduma za benki, wakati zaidi ya theluthi ya wakulima wadogo hawatamii huduma yoyote ya fedha.




Chanzo: jumla kuu ya watu wazima

Mikoa yenye kiwango kikubwa cha wasiotumia huduma za fedha



Msingi: jumla ya watu wazima kimkoa

Mikoa yenye kiwango cha juu cha wanaotumia huduma za kifedha



Msingi: jumla ya watu wazima kimkoa


Mkoa wa Kilimanjaro unabakia kileleni mwa jedwali la utumiaji wa huduma za fedha, japo unakaribiwa sana na Dar es Salaam iliyo kwenye nafasi ya ya pili. ilhali, watu wa Zanzibar na Singida wana viwango vya juu vya kutotumia huduma za fedha. Hata hivyo, kuna ongezeko la kasi la idadi ya watu katika mikoa yote linatumia huduma kwa simu za mkononi ndio maana upatinakaji wa bidhaa na huduma za fedha unaongezeka nchini kote.




KUTOTUMIA HUDUMA ZA KIFEDHA

Ni akina nani wenye uwezekano mkubwa zaidi wa kutotumia kabisa huduma za fedha?


Wale wenye uwezekano mkubwa zaidi wa kutotumia huduma za fedha ni vijana (hususan wa kike), wakulima, wenye kiwango cha chini cha elimu, na wale wanaowategemea wengine kifedha.




Watu wazima wa vijijini




Wanawake




Vijana (chini ya miaka 30)




Shule ya msingi au chini




Theluthi 2 za chini zaidi ya kiwango cha ustawi




Wakulima wa kujikimu/wadogo



Kilimo Biashara ya Kilimo




Wategemezi

 % ya wasiotumia huduma za fedha

Msingi: watu wazima wasiotumia huduma za fedha



Mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa Huduma za Fedha: Ulinganisho wa nchi mbalimbali



Msingi: jumla kuu ya idadi ya watu wazima (miaka 18 au zaidi) kwa kila nchi.

2009 charts have been recalculated using the 2013 definition of the Access Strand - Chati za mwaka 2009 zimekokotolewa upya kwa kutumia tafsiri ya mwaka 2013 za mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa Huduma za Fedha

Tanzania ina kiwango cha juu zaidi cha uwiano wa watu wanaotumia huduma rasmi za fedha kutoka taasisi zisizo benki kuliko nchi nyingine. Kupanda huku kwa nafasi ya ya Tanzania katika jedwali hili kumechangiwa zaidi na mtandao mkubwa wa utumiaji wa huduma za fedha kwa simu za mkononi. Hata hivyo, iwapo chanzo hiki hiki kingeondolewa na badala yake ingeangaliwa idadi ya watu wanaotumia huduma za benki peke yake, Tanzania ingeporomoka na kuwa karibu na Msumbiji kwenye jedwali.

UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA FEDHA


Upatikanaji kijografia

Kwa jumla, mikoa iliyo Kusini na Magharibi haina huduma nzuri za fedha kama maeneo mengine ya nchi. Karibu 40% ya watu wazima wako ndani ya umbali wa kilomita 5 kutoka tawi la benki, mashine za kutolea fedha benki, taasisi za huduma ndogondogo za fedha / Vyama vya Akiba na Mikopo au wakala wa huduma za fedha kwa simu za mkononi.




MATUMIZI YA HUDUMA RASMI ZA FEDHA

Kukua kwa sekta rasmi isiyo ya kibenki



Huduma za fedha kwa simu za mkononi zinavyotumika




Ingawa matumizi ya huduma za fedha kwa simu za mkononi - kwa kulipia bili, karo na kwa ajili ya miamala - kwa sasa bado yako chini, matarajio ni kwamba punde tu hili ndilo eneo litakalokuwa na kupanuka zaidi kuliko eneo lingine katika tasnia hii.. Pia, kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa huduma za akiba na mikopo zinazotumia simu za mkononi.

MATUMIZI YA HUDUMA RASMI ZA FEDHA

Wakati yamekuwapo mabadiliko madogo katika takwimu za vijijini kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, idadi ya watu wazima wanaotumia huduma za benki nchini kote imebaki kuwa ndogo. Ingawa wanaume wengi zaidi sasa wanatumia benki katika maeneo ya mijini, kasi ya ongezeko kwa wanawake ni ndogo zaidi. Kumekuwa na ongezeko la 5% kwa idadi ya watu wazima wanaotumia huduma za benki katika kila kundi rika, isipokuwa wale wa umri wa kati ya miaka 51-60.


Ni akina nani wanatumia benki?



Ni nini kinazuia watu wanaojishughulisha na kilimo kutumia bidhaa za benki? 29% ya wakulima ambao hawana akaunti za benki wanasema hawana mapato ya kutosha kuwa na akaunti ya benki; 20% wanasema hawawezi kumudu kiwango cha chini cha salio wakati 17% wanasema benki ziko mbali sana.

Msingi: jumla ya watu wazima kukotkana na chanzo kikubwa cha mapato

Watu wanatumiaje sekta isiyo rasmi?




Robo ya watu wazima nchini Tanzania hupata mikopo ya mali kutoka vyanzo visivyo rasmi, na wachache - karibu mara mbili ya idadi ya mwaka 2009 – hukopa pesa kwa njia zisizo rasmi.

Msingi: jumla kuu ya watu wazima


Chati zimekokotolewa upya kwa kutumia tafsiri za mpanuko wa upatikanaji na utumiaji wa Huduma Fedha za mwaka 2013

Matumizi ya huduma za fedha kwa simu za mkononi kwa Zanzibar na Bara

% ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha kwa simu za mkononi mwaka 2013



% ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha kwa simu za mkononi mwaka 2009



Kama ilivyoonekana, matumizi ya huduma za fedha kwa simu za mkononi yanachagiza upatikanaji wa huduma za fedha kwa upande wa Bara ambapo mmoja kati ya watu wazima wawili amejisajili. Hata hivyo, kasi ya watu wa Zanzibar kujihusisha na huduma hii ni ndogo zaidi; huko ni mmoja kati ya watu wazima watano anayenufaika na huduma za fedha kwa simu za mkononi.

Bara Zanzibar

Msingi: idadi jumla ya watu wazima kwa Bara na Zanzibar





HALI YA MWINGILIANO WA HUDUMA ZA FEDHA ZA FEDHA KATIKA SEKTA MBALIMBALI


Taratibu za usimamizi wa fedha

SEKTA ISIYO RASMI

SEKTA YA BENKI




SEKTA RASMI ISIYO YA BENKI



Chati hii inaonyesha suala la kuvutia kuhusu tabia ya kutumia huduma za fedha: benki zinatumiwa zaidi kwa ajili ya kuweka akiba, huduma rasmi zisizo za benki (mara nyingi ni kwa simu za mkononi) zinatumiwa kutuma fedha na sekta isiyo rasmi inatumika zaidi kwa ajili ya mikopo.

- % ya wanaotumia benki
- % ya watu wazima wanaotumia sekta isiyo rasmi
- % ya watu wazima wanaopata huduma rasmi zisizo za kibenki



Mwingiliano katika matumizi ya huduma rasmi na zisizo rasmi


Watu wengi wanatumia huduma mbalimbali kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi ili kukidhi mahitaji yao. Watu wazima milioni 5.4 wanatumia bidhaa na huduma rasmi zisizo za benki pekee, wakati milioni 5 wanatumia zote huduma rasmi zisizo za benki (hasa simu za mkononi) na utaratibu usio rasmi. Matumizi ya huduma za benki pekee yanabaki kuwa ni madogo.

WASITOTUMIA HUDUMA ZA FEDHA NI MILIONI 6.6

Msingi: jumla kuu ya watu wazima

MPANUKO WA UTARATIBU WA KUWEKA AKIBA

Watu huweka wapi akiba?



Msingi: Jumla kuu ya watu wazima


: Watu wengi huweka akiba nyumbani

Watu wazima walio wengi (39%) huamini kuwa kuweka akiba ni “kuhifadhi fedha mahali ambapo huwezi kuzipata kwa urahisi na kuzitumia mara unapozihitaji” na sio njia ya kujiongezea utajiri/rasilimali

Kupata fedha haraka ndiko kunakochochea uchaguzi wa njia ya kuweka akiba (ni kichocheo muhimu zaidi cha uchaguzi kwa mujibu wa 64.9%) ya waweka akiba

● % watu wazima 2013 ● % watu wazima 2009


Msingi: watu wazima wanaoweka akiba (kwa namna zaidi ya moja)




Inaonekana wazi kwenye chati hii kuwa licha ya kuwapo kwa njia tofauti, mahali maarufu zaidi pa kuweka akiba ni nyumbani. Ni dhahiri, idadi ya watu wazima wanaoweka akiba nyumbani kimeongezeka toka mwaka 2009. Kuna ongezeko dogo sana, lakini ambalo ni wazi katika kukua kwa idadi ya waweka akiba katika taasisi zisizo benki, hususan simu za mkononi (Ikijumuisha wanaoweka akiba kwa namna zaidi ya moja - siyo teng'anifu).

VIKWAZO VYA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA FEDHA


Vikwazo kwa huduma za benki




 % ya watu wazima wasiopata huduma za benki

Msingi: jumla kuu ya watu wazima wasiopata huduma za benki

Vikwazo vya huduma za fedha kwa kutumia simu za mkononi




 watu wazima wasiotumia huduma za fedha kwa simu za mkononi.

Msingi: Jumla kuu ya watu wazima wasiotumia huduma za fedha kwa simu za mkononi.


Vikwazo vya kupata huduma za benki na zile zisizokuwa za benki vinawazuia mamilioni ya watu kupata huduma za fedha. Ukosefu wa pesa, viwango vya juu vya salio la chini, uelewa mdogo wa masuala ya fedha na kuishi katika maeneo ya pembezoni bado yanaendelea kuwa ni miongoni mwa matatizo makubwa katika upatikanaji wa huduma hii.



Vikwazo katika huduma za bima



Vikwazo vya Kupata Mikopo



Miongoni mwa wasio na bima, wengi wao hawajawahi hata kusikia kuhusu huduma hii. Ambao wameshawahi kuisikia, wanaamini kuwa hawatamudu gharama zake, hawajui namna au mahali pa kupata huduma hiyo au hawaelewi jinsi inavyofanya kazi.

Kwa wale wasiokopa, sababu kubwa ni hofu ya kushindwa kulipa mkopo. Karibu nusu yao wanasema hawataki na wala hawahitaji kukopa.



HITIMISHO

Ushahidi kutoka Finscope Tanzania mwaka 2013 unaonyesha kuwa zipo sababu nyingi za kuwa na matumaini. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa watu wasiotumia kabisa huduma za fedha: mwaka 2009 watu milioni 11.7 walikuwa kwenye kundi hili la wasiotumia kabisa huduma za fedha, idadi ambayo imepungua kwa karibu nusu yake kufikia mwaka 2013. Sababu kubwa ya hali hii inayotia hamasa ni kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya huduma za fedha kwa simu za mkononi. Nusu ya idadi ya watu wazima - kiwango kilicho cha juu kuliko sehemu nyingine yoyote Afrika - wamejifunza namna ya kutumia mfumo huo na wanaendelea kunufaika na kupanuka kwa huduma zake.

Ijapokuwa matumizi yaliyozoeleka zaidi ya huduma za fedha kwa kutumia simu za mkononi ni kwa kutuma pesa, kukua kwa teknolojia na ubunifu kunaanza kuonyesha upatikanaji wa bidhaa na huduma mbalimbali zilizo salama, za kuaminika na nafuu. Makadirio yanaashiria kuwa, kwa miaka michache ijayo, watu wengi zaidi watatumia bidhaa na huduma za fedha kwa simu za mkononi kwa ajili ya aina mbalimbali zaidi za miamala ya fedha.

Kukua kwa uwanda wa huduma za bima na zinazobadilika kwa mujibu wa mahitaji kumesababishapelekea kuongezeka kwa umaarufu wa huduma hizo za fedha kwa kutumia simu za mkononi, ambazo kwa kiasi kikubwa zinahusiana na sekta ya afya. Watu wengi wanatumia bima kuzilinda familia zao dhidi ya gharama kubwa za huduma za afya na malipo ya tiba.

Matumizi ya bidhaa na huduma za benki hayaongezeki kwa kiasi kikubwa. Ingawa kuna ongezeko la kiwango cha kuweka akiba, watu wengi wanaohitaji huduma za mikopo huzipata huduma hizo kwenye sekta isiyo rasmi, na siyo sekta rasmi. Katika maeneo ya pembezoni, ambako watu wengi zaidi wanaishi, ndiko kunahitaji kuangaliwa kwa karibu zaidi. Benki zinahitajika kutatua haya matatizo haya ya , siyo tu lile la upatikanaji finyu wa huduma, pamoja na bali vilevile la suala la masharti na taratibu ngumu. Bidhaa na huduma mwafaka nyingi zaidi, hususan kwa ajili ya watu waishio katika maeneo ya pembezoni, zinahitajika ili utumiaji wa huduma jumuisi za fedha shirikishi uwe endelevu nchini Tanzania.

MAANA YA ISTILAHI

Wanaotumia huduma za Fedha	Watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi ambao wanamiliki/wanatumia bidhaa /huduma za fedha.
Wasiotumia huduma za Fedha	Watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi ambao hawatumii KABISA taratibu zozote za huduma za fedha - hujitegemea wenyewe/familia zao/marafiki kwa ajili ya kuweka akiba, kukopa na kutuma pesa; miamala yao hufanyika kwa kutimia pesa taslimu.
Wanaotumia huduma za fedha zilizo rasmi	Watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi ambao wanamiliki/wanatumia bidhaa /huduma za fedha zinazotolewa na watoa huduma wanaosimamiwa au walio chini ya muongozo rasmi.
wanaotumia huduma za Fedha zisizorasmi	

2006 / 2009

Makundi	Kiwango cha juu cha utumiaji huduma
Rasmi	Benki za biashara Benki ya Posta Bima
Rasmi kiasi	Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) Taasisi za Huduma Ndogondogo za Fedha Kampuni za utumaji fedha Huduma za Fedha kwa simu za mkononi
Zisizo rasmi	Kuweka akiba/vikundi vya mikopo Maduka/ Mikopo kwenye minyororo ya thamani Wakopeshaji binafsi Marafiki/familia
Wasiotumia	Kuweka akiba nyumbani/ kwa kununua rasilimali

KUNDI RIKA: Watu Wazima-miaka 16 zaidi

2013

Makundi	Kiwango cha juu cha utumiaji huduma
Za Kibenki	Benki za biashara Benki ya Posta
Rasmi-zisizo za Kibenki	Bima Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) Taasisi za Huduma Ndogondogo za Fedha Kampuni za utumaji fedha Huduma za Fedha kwa simu za mkononi
Zisizo Rasmi (za nje)	Kuweka akiba/vikundi vya mikopo Maduka / Mikopo kwenye minyororo ya thamani Wakopeshaji binafsi
Wasiotumia	Marafiki/familia Kuweka akiba nyumbani/ kwa kununua rasilimali

KUNDI RIKA: Watu Wazima-miaka 16 na zaidi

KUHUSU FSdT

Taasisi ya kuboresha Huduma za Fedha Nchini - The Financial Sector Deepening Trust (FSdT) imegharamia tafiti zote za FinScope nchini Tanzania kwa : miaka ya 2006 na 2009 na sasa 2013. Lengo la FSdT ni kujenga uwezo na uendeleu wa sekta ya fedha ili kukidhi malengo ya biashara za kwango cha chini, ndogo ndogo, na za kati (MSMEs,); na ya masikini - waume kwa wake kwa waume pamoja kuchangia katika kukuza uchumi. Hii ina nafasi muhimu katika kukuza uchumi.

FSdT imechangia katika mabadiliko ya huduma za fedha Tanzania, kama yanayoonekana kwenye utafiti wa mwisho wa FinScope, katika maeneo ya Mchango wa sera, sheria na taratibu; mazingira wezeshi; na utendaji wa watoa huduma.

FSdT ilianzishwa mwaka 2004. Kwa sasa inapata fedha kutoka kwa washirika watano wa maendeleo ambao ni: DFATD-Canada, DANIDA, SIDA, DFID pamoja na Mfuko wa maendeleo wa Bill na Melinda Gates. Kwa taarifa zaidi kuhusu FSdT, tafadhali ingia kwenye tovuti yetu: www.fsd.tz





facebook.com/FinScopeTZ



[@FinScopeTz](https://twitter.com/FinScopeTz)



Financial Sector Deepening Trust - Tanzania



FinScope
TANZANIA 2013



Ministry of Finance



Wadau



Watekelezaji



Wahisani